# GHARAMA YA MAFANIKIO



**SAID B. MAUMBA**
**Mwanzilishi wa MAUMBA BLOG**

# DODOSO

Mafanikio sio rahisi (cheap) bali ni gharama sana. Lakini je! ni kiasi gani upo tayari kulipia gharama kwa ajili ya ndoto zako na mafanikio yako? Sawa basi hizi hapa ni gharama za mafanikio yako unazopaswa kuwa tayari kulipia kama kweli unataka kufanikiwa.

## Soma zaidi....

# SURA YA TATU

## KUTENGENEZA MTANDAO IMARA ZAIDI

### Mafanikio ni CONNECTION

# PANUA NETWORK YAKO. TENGENEZA MTANDAO ZAIDI.

Tunapoongelea mtandao huwa napenda sana kuanza na kukupa mfano wa buibui, yani spider. Buibui hutega nyuzi zake/tandabui (cobwebs) kwanza kwa kiasi na mwendo mdogo mdogo. Haishii hapo bali kila siku huendelea kusuka nyuzi tu. Kila mara utamkuta yuko *busy* kuimarisha tandabui zake ambazo hutumia kunasa wadudu mbalimbali ambao bila shaka ndicho chakula chake kinachomuweka mjini!

Kwahiyo kadri mtandao wa tandabui za buibui unavyozidi kuwa imara zaidi ndivyo anaweza kunasa wadudu wengi zaidi. Na sio wengi tuu bali wakubwa zaidi, maana nyuzi huwa imara sana. Basi buibui anaendelea zake kuishi vizuri zaidi. Hiyo ndiyo faida ya mtandao imara… sio kwako tuu ambapo ndiyo nimepanga na ninaenda kuongelea bali hadi hapo nadhani umeona mwenyewe ilivyo na umuhimu hata kwa buibui.

Sasa naomba turudi kwako wewe!

## Kwani Unawezaje Kuunda Mtandao Imara Kwa Kupanua Network Yako Na Kutengeneza Connections Zaidi?

Ok! Ngoja kwanza nikuulize. Hivi si umewahi kusikia watu wanasema,

> *“Dunia ya sasa bila connection hutoboi.”*

Ni kweli wapo sahihi. Ila hapa nitakuelezea sasa njia kadhaa za kuijenga hiyo connection kutengeneza mtandao imara zaidi kwa ajili ya kukurahisishia kukutana na mafanikio yako. Na hapa ndipo ninapokumbuka kuna msemo niliwahi kuusoma sehemu ambao unasema,

> *“Kwenye mafanikio ya biashara au mafanikio yako binafsi hayategemei unafanya nini au una kipaji gani bali unajuana na kujulikana na nani?”*

Yani nani anajua hicho unachokifanya?

Kadri wengi wanavyojua unachokifanya basi kuna nafasi kubwa ya kuonekana na kukutana na watu sahihi. Na hapo ndipo ilipo siri ya mafanikio ambayo imekuwa wimbo wa taifa la MAFANIKIO. Ni wimbo mfupi sana unaosema…

> *"Ukitaka mafanikio, fanya kitu sahihi, mahala sahihi, na watu sahihi, ndani ya muda sahihi, katika namna au njia sahihi"*

Hiyo ndiyo kanuni mama ya mafanikio popote pale. Lakini sasa umeona hapo kwenye *watu sahihi*. Ni hapo ndipo uchawi wa connection unapoanzia. Yani itabidi ufanye juhudi na bidii ukutane na ujuane na watu wengi zaidi. *"Penye wengi, pana mengi"* lakini pia, hapakosi watu sahihi kwa ajili yako. Kwahiyo nafasi ya mtandao imara (Strong Network) ni muhimu sana kwenye safari ya mafanikio yako. Na nimedhamiria kukuelezea kwenye kurasa chache zinazofuata.

# SASA VIPI TUNAWEZA KUUNDA NA KUPANUA NETWORK ZETU?

Zipo njia nyingi sana kwa kweli. Lakini hapa nimechagua kukuelezea mbinu au njia takribani tano ambazo unaweza kutumia au tunaweza kutumia katika kukuza network yetu, katika kuunda connections zaidi itakayotusaidia kukutana na watu sahihi katika kitu tunachokifanya na kisha kufikia mafanikio.

## 1. MAWASILIANO KWANZA

Network inaanza pale unapobadilishana business card. Pale unapobadilishana nambari ya simu. Na pia pale unapomtajia mtu na kisha kubadilishana majina ya akaunti za mitandao ya kijamii au emails pia. Hapo kwa kweli ndipo mtandao au connections zinapoanzia.

Mawasiliano ndiyo yatakufanya uwasiliane na watu! Yani namaanisha, yatakuwezesha wewe kuwasilisha *mawazo (ideas)*, *mitazamo (Attitudes)*, *fikra (thoughts)*, *maono (vision)* vilevile kuonesha *uwezo (abilities)* na *vipaji (talents)* vyako kwa watu wengine. Lakini pia mawasiliano hayohayo yatakuwezesha wewe kufahamiana na watu zaidi na kujua *uwezo* wao, *mitazamo* yao, *umuhimu* wao na *fursa* kutoka kwao. Kwahiyo mawasiliano ni kama wembe. Una makali pande zote mbili. Yani yanawasaidia ninyi wote, sio wewe tu lakini vilevile mtandao wako.

Kuna kauli maarufu sana inasema,

> *"Your network, is your Networth"*

Sijui ushawahi kuisikia. Lakini…

# CHANGAMKIA OFFER LEO

## Hii offer ipo hivi

Ndani ya siku nne kuanzia, ikiwemo leo **25/06/2022 Jumamosi** hadi Tarehe 28 utalipia gharama ndogo malipo kabla, na utakipata kitabu hiki siku ya uzinduzi wake hapo tarehe **28/06/2022 Jumanne**. Ni ofa ya muda maalum na hivi ndivyo ilivyo:-

## Leo Jumamosi 25/06/2022 (Siku ya kwanza)

Bei ya leo ya offer ni **1,000** tu! Kwa ***kitabu hiki chenye thamani ya 11,000*** kitakapozinduliwa. Lakini Ukilipa hiyo, moja kwa moja nakutumia kitabu siku ya uzinduzi. Hakuna gharama ya ziada.

## Jumapili 26/06/2022 (Siku ya pili)

Bei ya offer inaongezeka na kuwa **1,500** kwa watakaolipa siku hii, moja kwa moja nakutumia kitabu siku ya uzinduzi. Hakuna gharama ya ziada.

## Jumtatu 27/06/2022 (Siku ya tatu)

Bei ya offer inaongezeka na kuwa **2,000** kwa watakaolipa siku hii, moja kwa moja nakutumia kitabu siku ya uzinduzi. Hakuna gharama ya ziada.

## Jumanne 28/06/2022 hadi saa 10 jioni (Siku ya nne)

Bei ya offer inaongezeka na kuwa **5,000** kwa watakaolipa siku hii, moja kwa moja nakutumia kitabu siku ya uzinduzi. Hakuna gharama ya ziada. ***Kuwahi Ndio Ujanja!***